


**AFYA**

Vifaa vya lishe bora vyajumuishwa kwenye orodha ya Dawa Muhimu 2019

UK 3



**BURUDANI**

KFCB kutathmini upya ada ya leseni ili kuvutia vijana kushiriki sanaa ya ubunifu

UK 4

**KILIMO**

Mradi wa maji kujisafirisha Tana River kukamilika Aprili



Uk 6

www.mygov.go.ke

JANUARI 31, 2023

TATHMINI YAKO YA WIKI

MyGov.

TOLEO No. 29/2022-2023

# KPA yatenga Sh2.1b kujenga bandari ya uvuvi ya Shimoni



Mwenyekiti wa KPA Benjamin Tayari asema kwamba ujenzi ambao umekuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu wa mradi wa Bandari ya Uvuvi ya Shimoni ni sehemu ya juhudi za serikali za kuinua uvuvi katika eneo la pwani

**NA HUSSEIN ABDULLAHI NA MARY ALUOCH (KNA)**

Mamlaka ya Bandari ya Kenya (KPA) has imetenga Sh2.1 bilioni kwa ujenzi wa mradi wa Bandari ya Uvuvi ya Shimoni katika kaunti ya Kwale.

Ujenzi wa bandari hiyo unatarajiwa kuwa na athari chanya kwa biashara na ukuaji wa uchumi kupitia uendelezaji mkubwa wa sekta ya uvuvi inayopigwa jeki na soko lilolo tayari na uongezaji thamani ambao utachochea uundaji wa maeneo spesheli ya uchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya KPA Benjamin Tayari alisema kwamba ujenzi ukisubiriwa kwa muda mrefu wa mradi wa Bandari ya Uvuvi ya Shimoni ni sehemu ya juhudi za serikali kuinua uvuvi katika eneo la pwani.

Tayari alisema kwamba kufikia sasa Sh2.5 bilioni zimetengwa kwa bandari hiyo ya kiviwanda ya uvuvi na akaongeza kuwa pesa zaidi zitatengwa kwa mradi huo wakati unaposonga.

ENDELEA UK 2

## KTDA kutengeneza chai iliyoongezwa thamani kuongeza mapato

**NA BERNARD MUNYAO (KNA)**

Shirika la Ustawi wa Chai Kenya (KTDA) limezindua mpango wa kusaidia utengenezaji wa chai halisi iliyoongezwa thamani katika viwanda vyake vyote nchini.

Mwenyekiti wa KTDA David Ichoho alisema kwamba itaweka mashine za kutengeneza chai hiyo katika viwanda kumi na vitatu maeneo tofauti nchini.

Akihutubia wakurugenzi wa viwanda vya chai kaunti ya Murang'a, Ichoho alisema kwamba serikali ya kitaifa iliahidi kutoa Sh800 milioni kusaidia katika ununuzi wa mashine za kutengeneza chai hiyo.

"Pesa hizo zitatusaidia kununua mashine nane huku shirika likinunua zingine tano ziwe kumi na tatu.

"Mashine hizo zitasaidia kutengeneza kutengeneza chai halisi ambayo mahitaji yake ni ya juu katika soko la kimataifa na ambayo hatimaye itawezesha wakulima kupata faida zaidi," alisema mwenyekiti huyo.

Ichoho alisema kwamba



ENDELEA UK 2

### Takwimu za Wiki

**2030**
Mwaka ambapo kaunti ya Kisumu imeazimia kumaliza kansa ya kizazi katika sehemu hiyo

**100,000**
Upungufu wa mchele kwa tani ambazo huagizwa kutoka nje

**20M**
Kilo za kahawa ambazo kaunti ya Murang'a kuzalisha licha ya kuwa na uwezo wa kukuza zaidi

**5,000**
Katoni za Vyakula Vilivyo tayari Kutumika ambavyo vilitolewa na WHO kwa Idara ya Afya ya Umma

**800M**
Kiasi cha pesa serikali itatoa kwa viwanda 13 vya majani chai kununua mashine za kuongeza thamani

**2,400**
Kadi za waandishi habari zilizotolewa na Baraza la Vyombo vya Habari ambavyo vitasitishwa kutumika

**2,000**
Wasimamizi wa TVETs ambao wamepewa mafunzo katika Kenya School of TVETs

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"

HOMA · KIKOHOZI · KUSHINDWA KUPUMUA · MAUMIVU KOONI · KUUMWA NA KICHWA

# KPA kutumia Sh2.1b kujenga bandari ya uvuvi ya Shimoni

ENDELEA KUTOK UK 1

Alifichua kwamba ujenzi wa miundomsingi ya bandari hiyo mpya ya uvuvi utafadhiliwa kwa kutumia pesa za KPA.

Bw Tayari alisema kwamba Kenya kwa wakati huu haina bandari mahususi ya uvuvi, na kwamba Bandari ya Shimoni, itakuwa na ukumbi wa soko, vifaa vya uhifadhi na kuweka dawa majitaka vitakavyokuwa vya kwanza nchini. Mkuu huyo wa KPA alisema kwamba wanawekeza pesa nyingi katika ujenzi wa miundomsingi ya bandari hiyo kuinua shughuli za uvuvi katika Bahari Hindi na kuvutia wawekezaji zaidi katika mfumo wa uongezaji thamani.

Tayari alisema kwamba fedha za kwanza zitatumiwa kwa awamu ya kwanza ya miundomsingi yakiwemo majengo, ujenzi wa barabara na kuondoa maji ya mvua katika bandari hiyo ya uvuvi.

> Tuko tayari kusaidia katika kuharakisha ujenzi wa bandari ya Shimoni,," -Achani



**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi KPA Benjamin Tayari akipokea hati ya shamba ya mradi wa bandari ya Shimoni kutoka kwa gavana wa Kwale Fatuma Achani afisini mwake.**

Akizungumza alipomtembelea Gavana wa Kwale Fatuma Achani, Tayari alisema kwamba mradi huo wa kimkakati ambao unapatiwa kipaumbele utachochea ukuaji wa sekta ya uchumi wa bahari.

Alisema kwamba bandari hiyo mpya ya uvuvi haitatumika kama injini ya kuendesha uchumi wa eneo la pwani, lakini pia utainua maisha ya maelfu ya wavuvi.

"Tunashukuru Rais William Ruto ambaye ameturuhusu kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Shimoni. Tayari tuko na mwanakandarasi katika eneo la ujenzi na tunataka kuhakikisha mradi huo unatekelezwa katika muda uliowekwa," akasema Tayari.

Alisema kwamba ujenzi wa bandari hiyo ya uvuvi ikiwemo vifaa vya uhifadhi na mashini za baridi utawezesha wavuvi wa eneo hilo kutumia bandari iliyo na vifaa vya kutosha na hivyo basi kuongeza thamani ya bidhaa za baharini.

Wakati wa ziara hiyo, Gavana Achani alimkabidhi mwenyekiti wa bodi hatimiliki ya Bandari ya Shimoni.

Aliahidi kuhakikisha ufanisi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Shimoni unaofanywa na KPA, ambao unatarajiwa kumalizika ndani ya muda wa miezi 24.

"Kama nchi, tuko tayari kutoa usaidizi wote unaohitajika kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Shimoni," alisema.

# KTDA kutengeneza chai iliyoongezwa thamani kuongeza mapato

ENDELEA KUTOKA UK 1

aina tofauti za chai halisi, ambazo zinajumuisha chai ya kijani kibichi, nyeupe au nyeusi zinahitajika mno na kwamba KTDA imetafuta soko ambalo linahitaji zaidi ya kilo milioni mbili kila mwaka dhidi ya uzalishaji wa humu nchini wa kilo 500,000.

Kwa wakati huu, viwanda vya KTDA zinatengeneza aina ya chai inayojulikana kama Cutting, Tearing na Curling (CTC) inayoleta mapato ya chini ikilinganishwa na chao halisi. "Mpango wetu ni kuongeza uzalishaji wetu wa chai halisi kwa sababu inahitajika kwa wingi na baadhi ya viwanda tayari vimenunua mashine zikitumia pesa zao wenyewe," alisema Ichoho.Alisema kwamba zaidi ya asilimia 95 ya chai inayozalishwa nchini inauzwa nje ya nchi na ni asilimia tano inayotumiwa nchini, jambo ambalo alisema, linaweka zao hilo kwa hatari ya kupungua kwa masoko ulimwenguni.Alitaja mfano wa msukosuko wa kisiasa unaoshuhudiwa katika nchi kama Pakistan na Iran ambazo ni baadhi ya zinazotumia chai ya Kenya kwa wingi. Afisa huyo aliongeza kuwa KTDA inalenga kutumia soko kubwa katika bara la Afrika.

Mwaka wa 2021, Kenya iliorodheshwa ya tatu miongoni mwa nchi zinazozalisha chai kwa wingi ulimwenguni baada ya China na Sri Lanka.

"Kama tutaweza kuondoa vizingiti vya ushuru na visivyo vya ushuru na kuzungumza na nchi binafsi, tutaweza kupanua soko letu," alisema.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alilalamikia uzalishaji duni wa chai ambao alihusisha na ukame unaoshuhudiwa nchini tangu mwaka jana. Kwa miezi sita iliyopita, Ichoho alisema nchi ilizalisha kilo 542,000 za chai ikilinganishwa na kilo 605,000 zilizozalishwa kati ya Januari na Juni 2022.

NCA
NATIONAL CONSTRUCTION AUTHORITY

## NOTISI YA TENDA WAZI YA KITAIFA

National Construction Authority (NCA) ni shirika la kiserikali chini lililoanzishwa chini ya sheria National Construction Authority Act 2011, kwa lengo la kusimamia sekta ya ujenzi na kushirikisha ustawi wake. Mamlaka inaalika maombi kutoka kwa washiriki kwa tenda zifuatazo;

| No | Nambari ya Tenda | Maelezo ya Tenda | Washiriki | Tarehe ya kufunguliwa/mwisho |
|---|---|---|---|---|
| 1. | NCA/T/010/2022-2023 | Utoaji wa huduma za tikiti za ndege | AGPO | Februari 8,2023 |
| 2. | NCA/T/011/2022-2023 | Utoaji wa Bima ya Personal Accident na Work Injury Benefit kwa wafanyakazi wa NCA | Mashirika ya Bima pekee | Februari 8,2023 |
| 3. | NCA/T/012/2022-2023 | Utoaji wa Bima ya Afya kwa Wafanyakazi wa NCA na wanachama wa Bodi | Mashirika ya Bima pekee | Februari 8,2023 |
| 4. | NCA/T/013/2022-2023 | Utoaji wa huduma za usafi katika Makao Makuu ya NCA na afisi za Supplies Branch | AGPO | Februari 8, 2023 |
| 5. | NCA/T/014/2022-2023 | Uuzaji wa mafuta na mafuta y kulainisha kwa magari ya NCA | Wazi | Februari 8,,2023 |

Stakabadhi za tenda zenye maelezo kamili na maekelezo zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya NCA; www.nca.go.ke na lango la Public Procurement Information, www.tenders.go.ke *bila malipo.*

**Manager Supply Chain**
**FOR: EXECUTIVE DIRECTOR**

@ncakenya | National Construction Authority | info@nca.go.ke | +254-0700 021 222

REPUBLIC OF KENYA
PUBLIC SERVICE COMMISSION KENYA

## PUBLIC SERVICE COMMISSION

**Our Vision**
*"A citizen-centric public service"*

**Our Mission**
*"To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery"*

## NAFASI YA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Maombi yaanalikwa kutoka kwa watu waliohitimu kujaza nafasi ifuatayo.

| V/NO. | CHEO | WIZARA/ IDARA YA SERIKALI | GREDI | IDADI YA NAFASI |
|---|---|---|---|---|
| 1/2023 | Mkurugenzi Mkuu, Public Investment and Portfolio Management | Hazina ya Kitaifa | CSG 3/Job Group 'U' | 1 |

Maelezo kamili kuhusu cheo yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya Tume.

Watu waliohitimu wanashauriwa kutuma maombi yao kwenye **MTANDAO** kupitia tovuti ya Tume: www.publicservice.go.ke au lango lkazi: www.psckjobs.go.ke

Public Service Commission imejitolea kutekeleza vipengelee vya Katiba-Sura ya 232 (1) kwa misingi ya haki, ushindani, uwakilishi wa makabila tofauti ya Kenya na kutoa nafasi sawa kwa wanaume na wanawake, pamoja na walemavu. **HIVYO BASI, WALEMAVU, WALIOBAGULIWA NA WALIO WACHACHE WANAHIMIZWA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yanapasa kufikia Tume mnamo au kabla ya **Februari 20, 2023 majira ya saa 11.00 jioni (saa za Afrika Mashariki).**

**Katibu/Afisa Mkuu Mtendaji**
**PUBLIC SERVICE COMMISSION**

KENYA VISION 2030

# Bidhaa za lishe sasa zimo kwenye orodha ya dawa muhimu ya Serikali

**NA JUDY SHERI (PCO)**

Wizara ya Afya, sasa imejumuisha bidhaa za lishe katika Orodha ya Kenya ya Dawa Muhimu 2019 hatua ambayo itawezesha KEMSA kununua na kuzihifadhi na kuzisambasa haraka kwa serikali za kaunti.

Kujumuishwa kwa bidhaa hizi ni sehemu ya juhudi za serikali za kutambua umuhimu wa bidhaa za kuokoa maisha kwa Wakenya katika kutimiza Afya kwa Wote (UHC).

Wizara pia imeanza mazungumzo na Wizara ya Fedha kuhusu hatua endelevu za mipango yake ya mikakati ambayo kwa wakati huu inafadhiliwa na washirika wa maendeleo..

Tangazo hilo lilitolewa na Katibu wa Idara ya Serikali ya Afya ya Umma na Viwango vya Utaalamu

Dkt Josephine Mburu alipopokea katoni 5000 za vyakula vya matibabu vilivyo



tayari kutumiwa (RTUF) za thamani ya Sh 26,389,440 kutoka kwa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO).

Mchango huo, ambao unatosha kutibu watoto

10,000 walio na umri wa miezi 6 hadi 59 walioathiriwa na utapia mlo hatari, utasaidia pakubwa juhudi za serikali kukabiliana na ukame unaoendelea katika maeneo yaliyo na uhaba wa chakula.

Dkt Mburu alisema kwamba lishe bora ni muhimu kwa ukuaji wa mtoto.

" Lishe ni muhimu hasa kwa afya ya watoto kwa kuwa inatekeleza jukumu muhimu katika ukuaji kuhakikisha mtoto ana afya ya kutosha, ni muhimu kwa watoto kula chakula kizuri kilicho na virutubishi aina tofauti," alisema Katibu.

Katibu alishukuru WHO kwa mchango huo na akasisitiza kujitolea kwa serikali kukabiliana na utapia mlo hasa katika kaunti 23 ambazo zimeathiriwa na ukame unaoendelea.

Dkt Mburu alifichua kwamba katika muongo



Dkt Josephine Mburu, katibu mkuu wa Aya alipopokea katoni 5000 za vyakula vya matibabu vilivyo tayari kutumiwa (RTUF)

mmoja uliopita, Kenya imepiga hatua kupunguza kiwango cha utapia mlo miongoni mwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano." Katika ripoti iliyotolewa majuzi ya Hali ya Afya Kenya, kudumaa kulipungua kutoka asilimia

26 mwaka wa 2014 hadi asilimia 18 mwaka wa

2022, kuwa uzani ulio chini ya unaofaa kulipungua kutoka asilimia 11 hadi asilimia 10 pekee.

Kulingana na utafiti huo, karibu watoto 1.13 milioni walio na umri wa chini ya miaka 5 wamedumaa; 315,066 hawakufikisha urefu na uzani wa wastani na 630,132 walikuwa na uzani wa chini 2022. Katibu aliongeza kuwa kaunti katika maeneo kame na nusu kame zimeathiriwa pakubwa na utapia mlo hatari kutokana na ukame unaoathiri utoshelevu wa chakula na shughuli za kujikimu kimaisha za jamii za eneo hilo.

"Uchanganuzi wa Utathmini wa Utapia mlo hatari (IPC AMN) uliofanywa Julai

2022 unaonyesha lishe nchini imedorora ikilinganishwa na msimu kama huo mwaka jana huku Turkana Kaskazini, Turkana Kusini na Laisamis zikikaribia awamu mbaya zaidi ambayo zaidi ya asilimia

30 ya watoto wako na utapia mlo. Hii ni sawa na watoto 884,464 walio na umri wa miezi 6 na 59 na akina mama wajawazito au wanaonyoshesha 115,725 ambao wanahitaji matibabu ya utapia mlo hatari," alisema.

ENGINEERS BOARD OF KENYA
Enhancing Professionalism

## NOTISI YA ZABUNI

Engineers Board of Kenya inaalika maombi kwa wanaopenda kushiriki tenda kutuma maombi kwa tenda zifuatazo:

| No | Marejeleo ya Tenda | Maelezo kuhusu Tenda | Washiriki | Tarehe na saa ya kufunga Tenda |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EBK/RFP/05/2022-2023 | Utoaji wa Huduma za Ushauri katika Utayarishaji wa Mpango Mkakatiwa (2023/2024 - 2027/2028) kwa Engineers Board of Kenya. | Wazi | Februari 28, 2023 saa 6.00 mchana. |

Mkusanyiko wa stakabadhi zote za tenda zapatikana kwa wanaotaka kutuma maombi baada ya kulipa **Sh1,000** kwa njia ya hundi ya benki au kuwekwa kwenye akaunti ya EBK katika National Bank of Kenya, Hill Plaza Branch Nambari ya Akaunti, 01001031539000. Ama, stakabadhi za tenda zinaweza kupatikana bila malipo kwenye tovuti ya EBK: www.ebk.go.ke au Public Procurement Information Portal: www.tenders.go.ke. Washiriki ambao wataamua kupakua stakabadhi lazima wawasilishe maelezo kuhusu kampuni yao kwa tenders@ebk.go.ke kunakiliwa au kupokea maelezo au ufafanuzi zaidi endapo utakuwepo.

Stakabadhi za tenda zilizojazwa na kuwekwa kwenye bahasha iliyoandikwa Nambari ya Tenda zinapasa kutumwa kwa:

**The Registrar/Chief Executive Officer**
**Engineers Board of Kenya**
**Fortis Suites, 9th Floor, Hospital Road, Upper Hill**
**P.O Box 30324-00100**
**Nairobi, Kenya**

Au kuwekwa kwenye Sanduku la Tenda lililoko kwenye sehemu ya kupokea wageni **Engineers Board of Kenya katika Fortis Suites 9th Floor, Hospital Road, Upper Hill** ili kupokelewa mnamo au kabla ya (tarehe za mwisho za kutuma tenda zimeonyeshwa hapo juu). Maombi ya tenda yatafunguliwa baada ya hapo katika chumba cha mikutano cha EBK mbele ya wawakilishi wa aliyetuma maombi ambao wataamua kuhudhuria.

**MSAJILI/AFISA MKUU MTENDAJI**
**ENGINEERS BOARD OF KENYA**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

KENYA WILDLIFE SERVICE

## MWALIKO WA ZABUNI

Shirika la Huduma kwa Wanyamapori Kenya lingependa kuwaalika Wagombea wa Kitaifa kwa zabuni zifuatazo:

| NO. | NAMBARI YA MAREJELEO | JINA LA ZABUNI | UHITIMU | DHAMANA (KES) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KWS/ONT/SEC/35/2022-2023 | UTOAJI WA HUDUMA ZA KUKATA, KUPIMA (CMT) NA KUSHONA | WAZI KWA WOTE (KAMPUNI ZA KUTENGENEZA NGUO) | 400,000/= |
| 2. | KWS/ONT/SEC/36/2022-2023 | UTOAJI NA USAMBAZAJI WA KOTI ZA MVUA | BIASHARA ZA WANAWAKE NA VIJANA | FOMU YA USALAMA WA ZABUNI |

Nyaraka za zabuni zilizo na maelezo ya kina na mahitaji zinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka kwa tovuti yetu; www.kws.go.ke na Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP), www.tenders.go.ke.

Waombaji wanaovutiwa wanaweza kutafuta maelezo zaidi kutoka kwa ofisi ya Uratibu wa Mfumo wa Usambazaji, Makao Makuu ya Shirika la Huduma kwa Wanyamapori Kenya, kati ya saa 8.00 asubuhi na 5.00 jioni wakati wa siku za kazi, **Simu. 020-2379407-15 Rununu: 0726610508/9**, au barua pepe: hps@kws.go.ke.

Ufafanuzi na/au marekebisho yote yatachapishwa kwenye tovuti ya KWS na wazabuni wanatakiwa kufanya hivyo tembelea tovuti iliyotajwa mara kwa mara katika kipindi cha zabuni kabla ya tarehe ya kufunga.

Zabuni zilizokamilishwa ziwekwe katika bahasha iliyofungwa iliyo na nambari ya marejeleo ya zabuni na jina la zabuni, zitawekwa kwenye **Sanduku la Zabuni** lililo kwenye **Lango Kuu la Mapokezi, Makao Makuu ya KWS, Barabara ya Langata P.O. Box 40241 - 00100, Nairobi mnamo au kabla ya tarehe 15 Februari 2023 saa 12:00 Adhuhuri.**

Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaotaka kuhudhuria katika Chumba cha Bodi ya Wanyama ya KWS.

Taarifa zaidi zinapatikana katika www.kws.go.ke.

**MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

KOMESHA COVID-19

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Serikali kutumia muundo msingi wake mkubwa wa ICT kibiashara

NA IRENE GALGALO (PCO)

Serikali hivi karibuni itaanza kupata thamani ya muundo msingi wake wa ICT kwa kuufanyia biashara kikamilifu na kuruhusu huduma zingine za serikali na sekta ya kibinafsi kunufaika nao.

Katika wa ICT na Uchumi Dijitali Mhandisi John Tanui, alisema kwamba idara hiyo inalenga kuinua sekta ya ICT nchini, kuhakikisha ulinzi wa data za kibinafsi kwa kuzingatia viwango vya dunia na kufanya huduma za serikali kuwa za dijitali.

Alikuwa akizungumza katika mahojiano na kituo cha runinga cha kitaifa.

Katibu alisema kwamba mchakato wa kugeuza huduma za serikali kuwa za dijitali unaendelea na Wizara ya ICT imewasiliana na idara zote kufahamu huduma zinazotoa ili kuwezesha Wizara kujua jinsi ya kuzifanya dijitali..

“Kwa sasa tunajenga uwezo wetu kuweza kujua ni rekodi ngapi na huduma zinazoweza kufanywa dijitali katika muda mfupi iwezekanavyo. Pia tunataka kutoa nafasi kwa wadau zaidi kuja na kusaidia kufanya huduma za serikali kuwa za dijitali. Safari ni ndefu lakini tunapanga kufanya huduma zote za raia kuwa za dijitali katika miezi sita,” alisema Katibu.

Idara hiyo ya serikali imethibitisha kwamba imekagua na kufahamu mali yote ya ICT ya serikali, mifumo na apu kutambua mapengo yaliyopo na maeneo yanayohitaji kushughulikia na tayari imeunda mfumo wa kukusanya data.



Katibu Tanui alisema Kenya na Afrika kwa jumula, ilikosa mageuzi matatu ya kiviwanda ambayo yalikuwa ya mpito wa uchumi lakini akasema kwamba mageuzi ya nne yanayoendelea ya kiviwanda ya tekinolojia ha dijitali kutumiwa kwa kazi, Kenya, itakumbatia nafasi zilizoko kwa vijana.

“Mpango wa serikali ni kuongeza kilomita 100,000 za nyaya za intaneti nchini kuhakikisha kwamba nafasi zinaweza kupatikana kutoka popote nchini. Vijana wetu wanaweza kupata kazi kupitia Huduma Zinazoweshwa na IT (ITES) ambazo wanaweza kufanyia kazi kampuni ya bara nyingine. Hatutaki kuwa watumiaji pia kuwa waundaji wa apu,” akasema Katibu.

# KFCB kuchunguza ada za leseni kuvutia vijana katika sanaa ya ubunifu

NA MUTISO MBITHI

Bodi ya Kuthibiti Filamu nchini (KFCB) itachunguza upya ada za leseni za sehemu zote za soko la sekta ya filamu nchini ili kuhimiza vijana kujiunga na uchumi wa ubunifu.

Bodi hiyo pia itahimiza wahudumu zaidi wa majukwaa ya kusikiza na kutazama ya “Video zinazohitajika zaidi na Zinazotazamwa zaidi” kujiunga na soko la humu nchini na kufungua nafasi mpya za kupata pesa kutoka kwa maudhui ya filamu na video zinazotengenezwa na vijana. Hii ni kwa kushirikiana na Wizara mlezi ya ICT na Uchumi Dijitali kuanzisha mfumo wa kujidhibiti wa wasanii wabunifu. Afisa Mkuu Mtendaji wa KFCB, Bw Christopher Wambua alisema mfumo kazi huo utarahisha ufanyaji biashara katika sekta ya filamu kwa kuhakikisha kwamba watangazaji na huduma za kibiashara za utiririshaji zitatathmini maudhui yao badala ya kuyawasilisha kwa bodi kukagua na kuweka viwango vya umri unaofaaWambua ambaye alikuwa akizungumza katika hafla ya kufunzu ya

Covid-19 na Uajiri Dijitali katika kituo cha AFRALTI, Nairobi alisema mfumokazi huo unalandana na lengo la mkakati wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali ya kuhakikisha wabunifu wanapata pesa kutoka kwa talanta zao, unaoitwa ‘Talanta Hela’.

REPUBLIC OF KENYA

## COMMODITIES FUND

COMMODITIES FUND
Financing Crops for Prosperity

## WE ARE ON THE MOVE!!!

Commodities Fund informs our clients, stakeholders and members of the public in general that **we have relocated** our Nairobi offices from Railways Headquarters to **UTALII HOUSE, 11th Floor** along **Utalii Street, off Uhuru Highway.**




The new office is within the Central Business District, Nairobi, hence easily accessible to our clients and stakeholders. From 1st February 2023, our new postal address is:

**Commodities Fund**
**Utalii House- 11th Floor,**
**Utalii Street , Off Uhuru Highway**
**P.O. Box 52714 -00200 Nairobi Kenya**

ComFund is a government agency under the Ministry of Agriculture & Livestock Development mandated to provide low cost financing to crops sector in Kenya. For farms operations, agro-processing/ value addition, working capital, access loans at an interest rate as little as 3% per annum!

***For further inquiries, email: info@comfund.co.ke; or call us: 0728 602427/8***
***Facebook: facebook.com/commoditiesfund; Twitter: @cofkenya***

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

GDC Geothermal Development Company
Green Energy for Kenya

## NOTISI YA ZABUNI

Kampuni ya Kustawisha Kawi ya Mvuke (GDC) inakaribisha zabuni kutoka kwa wagombeaji wanaostahiki kwa yafuatayo:

| NAMBARI YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | WATU LENGWA | DHAMANA | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| GDC/INFRA/OT/045/2022:2023 | Zabuni ya Ugavi na Ufungaji wa Mfumo wa Umeme Msaidizi wa Mfumo wa Usambazaji Maji wa Baringo Silali. | Wazi | Asilimia 2 ya jumla ya zabuni | 16/02/2023 saa 2:00 mchana |

Kutakuwa na **ziara ya Lazima** kwenye Kituo cha GDC cha Uendeshaji huko Baringo Silali kwa tarehe iliyo hapa chini kwa wazabuni wanaopenda katika Ratiba ya Kwanza (1) - Usambazaji na Uwekaji wa Jenereta na Transfoma;

**Maeneo ya Stesheni ya Pampu huko Baringo Silali (PS1 huko Chesiran, PS2 huko Paka & PS3 kwa Silali)** huko North Rift **Jumanne tarehe 7 Februari 2023 saa 9.00 asubuhi** (wakutane katika Ofisi ya GDC Kapkerwa (Kaunti ya Baringo) kando ya Barabara ya Marigat - Loruk saa 8.30am.) .

Wazabuni wanaohitajika wanaweza kupata maelezo zaidi na kukagua hati ya zabuni kutoka kwa afisi ya Meneja, Mfumo wa Usambazaji katika Kawi House, South C off Mombasa Road, Red Cross Road kati ya saa 9.00 asubuhi na 4.00 alasiri wakati wa siku za wiki.

Seti kamili ya nyaraka za zabuni inaweza kupatikana na mashirika yenye nia baada ya malipo ya ada isiyorejeshwa ya **Kshs.1000** inayolipwa kwa afisi yetu ya akaunti kwa pesa taslimu au kwa hundi ya benki.
Hati hizo pia zinaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.gdc.co.ke** au tovuti ya PPIP Portal **www.tenders.go.ke** ***bila malipo.*** Wazabuni wanaopakua hati ya zabuni kutoka kwa tovuti **LAZIMA** wapeleke maelezo yao mara moja kwa **procurement@gdc.co.ke** kwa rekodi na mengineyo na ufafanuzi wa zabuni na nyongeza.

Zabuni zilizokamilishwa katika bahasha zilizofungwa zilizoandikwa **Nambari ya Zabuni** na **jina la kumbukumbu la Zabuni**; zitumwe kwa:

**Mkurugenzi Mkuu na CEO,**
**Kampuni ya Kustawisha Kawi ya Mvuke**
**P.O Box 100746-00101**
**NAIROBI, KENYA**

na kuwekwa kwenye kisanduku cha zabuni katika Orofa ya Chini ofisi ya GDC Kawi House, South C kando na Mombasa Road, Red Cross Road kabla ya tarehe zilizotajwa hapo juu.

Zabuni zitafunguliwa mara moja baadaye mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika Kawi House, South C, Chumba cha Mikutano cha GDC, Orofa ya Chini.
Zabuni zilizochelewa hazitakubaliwa.

**MENEJA, MFUMO WA USAMBAZAJI**






# UNICEF yatoa dawa za kuokoa maisha kukabili milipuko kolera katika kaunti

**NA JUDY SHERI**

Serikali imetuma malori manne ya aina tofauti za bidhaa za afya, maji na usafi katika kaunti ili kusaidia kuzuia milipuko ya kolera ambao kufikia sasa umeripotiwa katika zaidi ya kaunti sita kote nchini.

Bidhaa hizo zilizotolewa na UNICEF, Ubalozi wa Ujerumani na washirika wengine zinanuiwa kuzuia athari mbaya za ukame ambao umekumba kaunti 23 na kuacha watoto zaidi ya 600,000 wakiwa na utapia mlo hatari. “Ninataka kuchukua fursa hii kutambua mchango mkubwa uliotolewa na marafiki wetu kama watu wa Jamhuri ya Ujerumani na washirika kama UNICEF, ambao wamechagua kutusaidia bila kuchoka,” alisema Waziri wa Afya Dkt Susan Nakhumicha Wafula alipokuwa akiaga malori hayo.

Kwa kipindi cha wiki 14 zilizopita, Wizara ya Afya imekuwa ikifanya juhudi kuzuia mlipuko wa kolera, ambao sasa umeathiri kaunti 14 kote nchini.

Waziri alifichua kwamba kupitia mchango wa marafiki na washirika, serikali imenufaika pakubwa na uimarishaji wa uwezo katika kukabiliana na dharura.

“Kufaulu kwa mchakato wa kushughulikia dharura, umefaulu pakubwa kutokana na ushirikiano mzuri ambao wizara imepata, ikiwemo usaidizi wa kiufundi katika mafunzo, usambazaji wa chanjo na bidhaa zingine za matibabu, ,” alisema Waziri.

**600,000**

**Watoto walio na utapiamlo katika kaunti**

Kando na mlipuko wa kolera, Waziri alisema kwamba Wizara imeendelea kushuhudia vitisho vingine vya afya kama vilivyozuiwa vya Ugonjwa wa Virusi vya Ebola (EVD) nchini Uganda na akahimiza nguvu kuelekeza kwa ufuatiliaji na maandalizi ya kukabiliana na hali ikitokea.

Waziri alishukuru timu za maandalizi ya kukabili ugonjwa wa Ebola na washirika kama UNICEF na Jamhuri ya Ujerumani kwa kuhakikisha ufuatiliaji uliimarishwa kwa kipindi cha miezi minne ambacho nchi ilikuwa katika hatari ya kukumbwa na mlipuko. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Maeneo Kame na Ustawi wa Kanda

Bi Rebecca Miano, Balozi wa Amerika nchini Sebastian Groth na Mwakilishi wa UNICEF Kenya Shaheen Nilofer.


# Mamlaka ya Kitaifa ya Kusimamia Mazingira

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

**Popo Road, off Mombasa Road P.O.BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya,**
**Simu: 0724253398, 0735013046 B/Pepe: dgnema@nema.go.ke Tovuti: www.nema.go.ke**

## TAARIFA KWA UMMA KUWASILISHA MAONI KUHUSU RIPOTI YA UTATHMINI WA ATHARI ZA MAZINGIRA KWA MRADI UNAOPENDEKEZWA WA HUDUMA YA MAJI BWAWA LA NDARUGO II KATIKA MTO NDARUGO NDANI YA ENEO LA THENGE-INI, NJE YA BARABARA YA THENGE-INI, KAUNTI YA KIAMBU

Kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Usimamizi na Uratibu wa Mazingira (Tathmini ya Athari na Ukaguzi), 2003, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) imepokea Ripoti ya Utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mradi uliopendekezwa hapo juu.
Mtetezi,, Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Athi, inapendekeza kujenga bwawa (lenye mwinuko wa crest wa 1800.00 m, upana wa crest wa Sm, urefu wa bwawa wa takriban 52m, urefu wa jumla wa 300m, eneo la mifereji ya maji linalodhibitiwa la 67. Km2, uwezo mzuri wa kuhifadhi wa m3 milioni 16.249, wastani wa usambazaji wa maji kwa mwaka wa m3 milioni 16.62, njia ya kumwagika, ulaji wa maji, sehemu ya chini na vifaa vinavyohusika), bomba la usambazaji wa maji (bomba la kugeuza, bomba la kusambaza, hifadhi na vifaa vinavyohusika) na kiwanda cha kusafisha maji chenye uwezo wa 50,000 m3/d kando ya Mto Ndarugo ndani ya eneo la Thenge ini katika Kaunti ya Kiambu.

Zifuatazo ni athari zinazotarajiwa na hatua za kupunguza zinazopendekezwa:

| Athari za Kimazingira/Kijamii | Mapendekezo ya Hatua za Kupunguza |
|---|---|
| Migogoro inayotokana na upotevu wa ardhi, maendeleo n.k., nyumba na mazao | • Fidia kwa watu walioathirika<br>• Kufahamisha wanajamii wote kando ya njia za bomba la<br>• mradi uliopendekezwa.<br>• Kujumuisha maoni ya jamii<br>• Uundaji wa ofisi ya mawasiliano ya jamii. |
| Kupotea kwa mimea | • Uhifadhi wa mimea inapowezekana.<br>• Tahadhari itachukuliwa ili kupunguza uharibifu wa kifuniko cha mimea kwenye njia ya bomba |
| Mmomonyoko wa udongo | • Udongo wa upotevu utakaotumika kujaza maeneo yaliyochimbwa/kusumbua<br>• Udongo wa kupoteza unapaswa kuunganishwa na roller ya mitambo ili kupunguza mmomonyoko wa upepo au maji |
| Kuongezeka kwa uzalishaji wa taka | • Tupa taka kwenye tovuti zenye leseni za kutibu taka kupitia vidhibiti taka vilivyo na leseni<br>• Kuzingatia kanuni za usimamizi wa taka za 2006 |
| Usumbufu wa trafiki barabarani | • Zingatia mazoezi mazuri ya kuendesha gari yanayopaswa kufuatwa<br>• Makutano / sehemu za ufikiaji zinazofaa zitatolewa<br>• Matumizi ya alama zinazofaa na zinazosomeka<br>• Ajira ya bendera rasmi / wanawake ili kuhakikisha usalama wa umma |
| Athari kwa utamaduni, maeneo ya kidini na nyeti | • Kuchora ramani za tovuti za kitamaduni, kidini na nyeti zinazoelekeza tovuti kwenye tovuti zisizo nyeti sana<br>• Kushauriana na wazee wa eneo na fidia kwa uharibifu wowote unaosababishwa |
| Matatizo ya ubora wa hewa | • Punguza viwango vya vumbi kupitia mazoea mazuri kama vile kumwagilia maji kwenye barabara za kuingilia, maeneo ya ujenzi, mikengeuko na maeneo mengine yenye usumbufu na kufunika lori zinazosafirisha vifaa vya ujenzi.<br>• Wape wafanyikazi vifaa vya kinga vya vumbi vinavyofaa ikiwa ni pamoja na barakoa na ovaroli<br>• Huduma ya mara kwa mara ya magari |
| Kelele na mitetemo | • Vizuizi vya kawaida kwa saa za kazi ya tovuti (8:00AM-5:00PM) na kuinua viunzi kwenye vifaa vya ujenzi.<br>• Matumizi ya vifaa vya kujikinga vya kusikia kama vile viziba masikioni na vimimina sauti vya masikio miongoni mwa wafanyakazi wakati viwango vya kelele vinapozidi 85-90dBA. |
| Hatari za Afya na Usalama | • Kubuni na kutekeleza hatua za usalama na mipango ya dharura ili kudhibiti hatari za ajali<br>• Weka alama za barabarani zinazofaa, alama na samani za barabarani<br>• Wape wafanyikazi mavazi ya kinga (vifuniko vya pua na mdomo, vifuniko vya masikio, ovaroli, buti za viwandani na glavu) na helmeti. |

| Athari za Kimazingira/Kijamii | Mapendekezo ya Hatua za Kupunguza |
|---|---|
| Masuala ya maji | • Angalau 30% ya mtiririko msingi unapaswa kutiririka kila wakati kwenye mkondo ili kudumisha mahitaji ya kiikolojia na kijamii chini ya mkondo<br>• Fuatilia athari za bwawa kwenye bonde la mto kwa wakati |
| Upotevu wa maji | • Maelezo ya kijiolojia yaliyopendekezwa kwa mafuriko yanapaswa kuanzishwa ili kutambua maeneo ya udhaifu na hatua zinazofaa za kuimarisha kuingizwa<br>• Mitindo ya upenyezaji wa maji chini ya uso kwenye maeneo yaliyoathiriwa inapaswa kuanzishwa na kufuatiliwa kwa muda kwa kuzingatia athari kwenye nyumba na miundo mingine.<br>• Panda miti na vichaka vya kiasili kuzunguka eneo la buffer la bwawa ili kupunguza upotevu wa maji kupitia michakato ya uvukizi. |
| Kuongezeka kwa uzalishaji wa maji taka | • Kuhakikisha kuwa kaya, taasisi na biashara zote zilizounganishwa kwenye mtandao mpya wa bomba la maji zimeunganishwa kwenye njia mpya ya maji taka inayopendekezwa ya manispaa.<br>• Maji taka yanapaswa kutibiwa kabla ya kutupwa |
| Athari za mabadiliko ya hali ya hewa | • Jumuisha athari za mabadiliko ya hali ya hewa kama vile joto kali na mafuriko katika muundo wa mradi<br>• Wafanyakazi wapewe vifaa vya kutosha na PPEs kwa ajili ya faraja katika kesi ya joto kali<br>• Jengo lijengwe kwa mifumo ya mifereji ya maji ya kutosha ili kudhibiti mafuriko<br>• Mshauri anashauriwa kujenga majengo na vifaa vinavyoweza kuhimili tetemeko la ardhi (tafuta ushauri zaidi kutoka kwa idara ya serikali ya jiolojia) |

1. **Katibu ,**
   **Wizara ya Mazingira na Misitu,**
   **Jengo la NHIF, Orofa ya 12,**
   **Barabara ya Ragati, Upper Hill,**
   **P.O.BOX: 30126-00100,**
   **NAIROBI**

2. **Mkurugenzi Mkuu, NEMA**
   **Popo Road, off Mombasa Road,**
   **P.O. BOX 67839-00200,**
   **NAIROBI**

3. **County Director of Environment**
   **KIAMBU COUNTY**

Nakala ya ripoti ya EIA inaweza kupakuliwa katika **www.nema.go.ke**

NEMA inawaalika wananchi kuwasilisha maoni ya mdomo au maandishi ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa notisi hii kwa Mkurugenzi Mkuu, NEMA, ili kusaidia Mamlaka kufikia mchakato wa kufanya maamuzi ya mradi huu. Tafadhali nukuu kumbukumbu Namba. **NEMA/EIA/5/2/2052.**

Maoni yanaweza pia kutumwa kwa barua pepe kwa **dgnema@nema.go.ke**

**MKURUGENZI MKUU**

***Tangazo hili limefadhiliwa na mtetezi***

ISO 9001 BUREAU VERITAS Certification
**National Environment Management Authority - Kenya**
**@NemaKenya**
KENYA VISION 2030

**“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**




# Mradi wa mabilioni wa kutumia nguvu za ardhi Tana kuisha Aprili

**NA SADIK HASSAN**

Mradi wa Mpango wa Unyunyuzaji na Ukarabati wa Bura ambao utabadilisha mradi wa unyunyuzaji wa Bura kutoka mfumo wa kupiga maji kwa pampu hadi mfumo wa uvutaji utakamilika Aprili mwaka huu. Hili kukamilisha kwa muda uliowekwa, Mamlaka ya Kitaifa ya Unyunyuzaji (NIA) imeweka mradi huo wa utoshelevu wa chakula wa gharama ya Sh 7 bilioni, ambao umechukua miaka 10 tangu ulipoanzishwa, chini ya mpango wa miradi inayofaa kukamilishwa katika siku 100.

Afisa Mkuu wa Shughuli wa NIA Joel Tanui alifichua kuwa mwanakandarasi amekamilisha asilimia 90 ya kazi katika mfumo huo, na akahakikisha kwamba mradi huo utakuwa umekamilika ndani ya miezi mitatu ijayo.

“Ni mmoja wa miradi ambayo tumeweka chini ya RRI. Tumeweza kutatua changamoto ambazo zilikumba mradi kuhusiana na mipangilio ya kandarasi na mwanakandarasi ambaye anaendelea na kazi. Tumekubaliana kwamba mwanakandarasi anafaa kukabidhi mradi huo ili uweze kunufaisha wakulima wa mradi wa Unyunyuzaji wa Bura,” alisema Tanui.

Akizungumza alipozuru mradi wa Unyunyuzaji



wa Tana, , Tanui alisema kwamba mradi huo unahusu ukarabati wa kazi ya unyunyuzaji, utoaji wa vifaa, ushauri na mikopo ili kuwa na unyunyuzaji wa kutegemea wa ekari 15,000 zaidi za ardhi.Mradi huo utahakikisha upatikanaji wa maji ya kunyunyiza kwa kasi ya lita 11,000 kwa sekunde mwaka mzima kinyume na lita 2,700 kwa sekunde kwa wakati huu.

# Nakuru yakumbatia tekinolojia mpya kupunguza hasara ya maji

**NA ESTHER MWANGI NA CHARLOTH CHEPKEMOI (KNA)**

Serikali ya kaunti ya Nakuru imewekeza katika tekinolojia mpya ikiwemo mabomba mapya ya kisasa na mita bora za kisasa kupunguza maji yasiyoiletea mapato kutoka kwa kampuni zake tatu za huduma za maji (WSPs).

Hii inanuiwa kupunguza uharibifu wa maji na kuimarisha uendelevu wa uchumi na uwepo wa maji katika kaunti hiyo.

Maji isiyoleta mapato (NRW) ni maji inayopotea kupitia uungwanishaji kinyume cha sheria au kupitia mita zizozofanya kazi. Bodi ya Kudhibiti Huduma za Maji (WASREB) inataja NRW ya asilimia 20 kama nzuri, asilimia 20-25 kama inayokubalika na zaidi ya 25 kama isiyokubalika. Waziri wa Maji, Mazingira, Kawi, Mali Asili na Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Nakuru, Dkt Nelson Maara alisikitika kuwa nchi inapoteza karibu lita 430,000,000 milioni za maji sawa na Sh12.2 bilioni, kila mwezi kutokana na uharibifu usiofaa na akasema kwamba serikali ya kaunti inanuia kupunguza viwango vya maji yanayoharibiwa kutoka asilimia 54 hadi asilimia 20 jambo ambalo litasaidia kuondoa uhaba wa utendaji bora katika mifumo na usambazaji maji na kuokoa pesa nyingi za umma.

Dkt Maara alisema kwamba ukaguzi wa NRW

**430,000**

**Lita za maji ambazo hupotea kila mwaka**

ulifichua kwamba kampuni hizo tatu za maji hupoteza zaidi ya nusu ya maji ya kunywa inayowekwa dawa kupitia uvujaji, wizi na mita mbaya, na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh 40 milioni kila mwezi na uhaba wa bidhaa hiyo.

Hata hivyo alisema mipango inaendelea kukarabati na kuboresha mifumo ya zamani ya kuweka dawa majitaka, usambazaji wa maji na maji taka inayosimamiwa na kampuni hizo tatu za maji ikiwemo Kampuni ya Huduma za Maji na Usafi ya Nakuru (Nawassco), Kampuni ya Maji na Usafi ya Maji Sehemu za Mashambani (Naruwasco) na kampuni ya Maji, Majitaka na Usafi ya Naivasha (Naivawasco), hatua ambayo alisema, inalenga kuhakikisha maji salama na ya kutosha ya kunywa.

# Baraza la Habari lafuta kadi za zamani kuondoa waandishi feki

**NA JANE GICHARU**

Baraza la Vyombo vya Habari la Kenya (MCK) limebatilisha kadi za wanahabari lililotoa mwaka huu na kuanzisha mpya ambazo zina sehemu za usalama.

Baraza limekusanya kadi 2,400 za wanahabari ambazo lilikuwa limetoa mwaka huu na litatoa zingine mpya bila malipo zaidi kwa wanahabari walioathiriwa au kampuni za habari.

Mahitaji mengine yanayonuiwa kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa wanahabari ni uamuzi wa wanahabari wa kujitegemea kujiunga na shirika la habari au chombo cha habari ambalo litatoa barua ya kuwapendekeza kabla yao kupatiwa kadi za uanahabari.

Kufuatia hatua hiyo mpya, duru za habari zimeshauriwa kuthibitisha uhalali wa wanahabari wanaohudhuria hafla zao kwa kutumia nambari maalumu katika kadi zao, alama ya siri inatoa jibu upesi (QR) au arafa ya kuthibitisha ya 40314 ili kuhakikisha wanashughulika na wanahabari wa kweli.

Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Vyombo vya Habari Bw David Omwoyo anasema kwamba baraza linatafuta njia za kumaliza matapeli ambao wamekuwa wakilaumiwa kwa kunyanyasa duru za habari kwa kuitisha pesa.

Bw Omwoyo alikuwa akizungumza katika mkutano wa wadau ulioitishwa na Baraza la Habari jijini Nairobi kujadili suala hilo la kuondoa matapeli kutoka sekta ya habari.

Wadau waliohudhuria walijumuisha wawakilishi kutoka Huduma ya Polisi Kenya, Mahakama, Chama cha Wanahabari Kenya (KUJ), Chama cha Wanahabari wanawake cha Kenya (AMWIK) na mashirika kadhaa ya habari.

Omwoyo alisema baadhi ya wanahabari wanaohangaisha ni watu waliokuwa wakifanya kazi katika vyombo vya habari lakini wakapofutwa kazi hivi majuzi mashirika yalipopunguza wafanyakazi.

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## MWALIKO WA ZABUNI

Kenya Power inakaribisha zabuni kutoka kwa wazabuni ili kutoa yafuatayo:-

| NO. | NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | TAREHE YA KUANZA | MKUTANO KABLA YA ZABUNI | TAREHE YA KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KP1/9A.3/OT/21/22-23 | Usambazaji wa Vifaa tofauti kwa marekebisho ya transfoma | Jumanne 31.01.2023 | Thursday 09.02.2023 at 10.00 a.m. **(Stima Plaza, Auditorium)** | Alhamisi 16.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 2. | KP2/9A/OT/01/22-23 | Ujenzi uliopendekezwa wa Mini Go-Down katika Machakos Store Yard | Jumanne 31.01.2023 | Jumatano 08.02.2023 saa 10.00 asubuhi (Kituo kidogo cha Machakos KPLC) | Jumanne 21.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 3. | KP1/9A.2/OT/036/CS/22-23 | Ununuzi na Uajiri wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Kidijitali | Jumatano 01.02.2023 | Jumatano 08.02.2023 saa 10.00 asubuhi **(Stima Plaza, Auditorium)** | Jumanne 21.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 4. | KP1/9A.3/OT/015/22-23 | Usambazaji wa vifaa vya Matangazo kwa Nguvu Kubwa na Huduma za Wateja wa SME na Uchapishaji kwa Msingi wa Maarifa (FAQS) | Jumatano 01.02.2023 | N/A | Jumanne 28.02.2023 saa 11.00 asubuhi |
| 5. | KP1/9A.2/OT/039/ICT/22-23 | Ununuzi wa Kompyuta na Vipakatalishi | Jumatano 01.02.2023 | N/A | Jumatano 22.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 6. | KP1/9A.2/OT/033/ICT/22-23 | Ununuzi wa Mkataba wa Uboreshaji na Matengenezo wa Neplan | Jumatano 01.02.2023 | N/A | Jumanne 21.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 7. | KP1/9A.2/OT/040/ICT/22-23 | Usambazaji, Usakinishaji, Usanidi wa Seva za Hifadhi Nakala za Vyombo vya Habari | Alhamisi 02.02.2023 | N/A | Alhamisi 23.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 8. | KP1/9A.2/OT/038/ICT/22-23 | Utoaji wa Vipuri kwa Uendeshaji na Matengenezo ya Mfumo wa SCADA/EMS | Ijumaa 03.02.2023 | Ijumaa 10.02.2023 saa 10.30 asubuhi **(Stima Plaza, Auditorium)** | Ijumaa 24.02.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 9. | KP1/9A.2/OT/022/ICT/22-23 | Provision of maintenance of UPS and LV Switchgear for Disaster Recovery Centre, Electricity House, Nairobi and Data Centre Stima Plaza | Friday 03.02.2023 | N/A | Thursday 23.02.2023 at 10.00 a.m. |

Nyaraka za zabuni zinazoelezea mahitaji ya zabuni zilizo hapo uu zinaweza kupatikana kutoka kwa tovuti ya Kenya Power (www.kplc.co.ke) kuanzia tarehe zilizoonyeshwa juu.

**MENEJA MKUU**
**MFUMO WA USAMBAZAJI NA VI-**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy
www.kplc.co.ke @Customercare.kplc.co.ke Kenya Power @KenyaPower 97771 0703-070 707, 0732-170 170

# TRA TOURISM REGULATORY AUTHORITY

~ Championing Quality and Excellence ~

## MWALIKO WA TENDA

